22112841

International Baccalaureate®
Baccalauréat International
Bachillerato Internacional

SWAHILI *AB INITIO* – STANDARD LEVEL – PAPER 1
SWAHILI *AB INITIO* – NIVEAU MOYEN – ÉPREUVE 1
SWAHILI *AB INITIO* – NIVEL MEDIO – PRUEBA 1

Friday 13 May 2011 (afternoon)
Vendredi 13 mai 2011 (après-midi)
Viernes 13 de mayo de 2011 (tarde)

1 h 30 m

TEXT BOOKLET – INSTRUCTIONS TO CANDIDATES

- Do not open this booklet until instructed to do so.
- This booklet contains all of the texts required for Paper 1.
- Answer the questions in the Question and Answer Booklet provided.

LIVRET DE TEXTES – INSTRUCTIONS DESTINÉES AUX CANDIDATS

- N'ouvrez pas ce livret avant d'y être autorisé(e).
- Ce livret contient tous les textes nécessaires à l'Épreuve 1.
- Répondez à toutes les questions dans le livret de questions et réponses fourni.

CUADERNO DE TEXTOS – INSTRUCCIONES PARA LOS ALUMNOS

- No abra este cuaderno hasta que se lo autoricen.
- Este cuaderno contiene todos los textos para la Prueba 1.
- Conteste todas las preguntas en el cuaderno de preguntas y respuestas.

© International Baccalaureate Organization 2011

KIFUNGU A

MWALIKO:

SAUTI ZA BUSARA – ZANZIBAR

Kila mwaka kuna sherehe nyingi za utamaduni katika kisiwa cha Zanzibar. Sherehe nzuri inayovutia kuliko zote ni hii inayoitwa SAUTI ZA BUSARA. Hii ni sherehe ambayo inakuwa pamoja na ile ya filamu mbalimbali ambazo zinaonyeshwa kwa wiki moja. Kwa kawaida vikundi kama vile vya Taarab, muziki wa dansi, Bongofleva, na vinginevyo hushindana, na zawadi kubwa ya pesa na cheti cha heshima hutolewa kwa mshindi. Mwaka ujao, SAUTI YA BUSARA itafanyika tarehe 11 hadi 16 Februari, na itashirikisha wanamuziki mbalimbali kutoka Tanzania na nje ya Tanzania. Kama unataka kushiriki katika sherehe hii unaweza kutuandikia kwa anuani ya Busara, S.L.P 3635, Zanzibar, Tanzania. Kama unataka kujua habari za sherehe hii unaweza kutembelea tovuti yetu ya www.busaramusic.org, au simu namba +255 773 822 294. Wote mnakaribishwa.

Wizara ya Habari Zanzibar, kutoka *Ijue Zanzibar* (Februari 2010)

KIFUNGU B

MASHINDANO YA MAONYESHO YA MAVAZI



Hivi karibuni kutakuwa na maonyesho na mashindano ya mavazi mbalimbali kutoka Tanzania, Kenya na Uganda. Mashindano hayo yatafanyikia mjini Dar es Salaam katika Ukumbi wa Mlimani City, karibu na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Maelfu ya watu watahudhuria na kuona mitindo mbalimbali ya mavazi. Pia wanamuziki kama vile AY, Banana Zorro, Chameleon, Juliana, Amani, Keisha, Mwasiti, Ray C, Lady Jaydee, Vumilia, Diamond, Fresh Jumbe, na wengine wengi watasindikiza maonyesho na mashindano hayo.

Kiingilio kitakuwa ni shilingi 5000 tu za Tanzania. Siku hiyo hiyo kutakuwa na mashindano ya mavazi ili kumpata msichana na mvulana aliyevaa vizuri kuliko wote. Zawadi kemkem na nzuri zitatolewa kwa washindi.

Tarehe kamili za mashindano zitatangazwa katika gazeti lako ulipendalo la *Kitangoma*. Watu wote wenye zaidi ya miaka 16 mnakaribishwa kuona mashindano ya muziki, na kushiriki katika mashindano ya mavazi. Ijapokuwa tunawapenda sana watoto, lakini kwa mashindano na maonyesho haya tafadhali watoto wasiletwe kwa sababu ni matukio kwa ajili ya watu wazima tu.

Kutoka *Kitangoma* (Machi 2010)

KIFUNGU C

MICHEZO NI UHAI

Mchezo wa mpira wa miguu ndio unaopendwa kuliko michezo mingine yote hapa Afrika na nadhani duniani kote. Yafuatayo ni mahojiano kati ya Dilunga, mwanasoka maarufu kutoka Tanzania, na mwandishi wa habari wa gazeti la kila siku la *Michezo Yetu*:

Mwandishi: **Habari zako Dilunga?**

Dilunga: Nzuri sana bwana mwandishi. Ninashukuru sana kwa kunikaribisha kwa mahojiano.

Mwandishi: **Hebu tuanze mwanzo kabisa. Ulizaliwa wapi na ulianzaje kupenda michezo mpaka umekuwa maarufu sana?**

Dilunga: Nilizaliwa huko Kilimanjaro, na tangu nilipokuwa mdogo nilipenda sana michezo. Tulikuwa tunacheza michezo mingi sana, pamoja na kukimbia, kujificha, rede, na zaidi soka au mpira wa miguu. Mimi nilipenda sana mpira wa miguu kwa sababu baba yangu pia alikuwa mcheza soka.

Mwandishi: **Ilikuwaje mpaka ukawa nyota wa mchezo huu?**

Dilunga: Nilipokuwa sekondari, tulifanya mashindano ya shule mbalimbali. Wakati wa mashindano hayo nilionyesha kipaji mchangu cha soka. Ndipo nilipochukuliwa nikachezea timu ya mkoa. Baadaye niliingizwa kwenye timu ya taifa. Nilichezea timu hiyo kwa muda mrefu sana, na tulitembelea sehemu mbalimbali duniani.

Mwandishi: **Unawaambia nini vijana wa leo kuhusu michezo, na hasa kuhusu mchezo wa soka?**

Dilunga: Michezo ni uhai. Ni muhimu kucheza na kufanya mazoezi kwa ajili ya afya zetu, lakini pia kwa ajili ya kupata furaha. Mtu akiamua kufanya mchezo fulani, afanye kwa moyo wake wote. Kwa njia hii atajikuta anafanikiwa sana.

Mwandishi: **Asante sana bwana Dilunga kwa kutupa mawazo yako kuhusu maisha yako na pia kuhusu michezo.**

Kutoka *Michezo Yetu Jumamosi* (Julai 2010)

KIFUNGU D

SAFARI! SAFARI!

Hizo hapo chini ni picha na habari za safari katika kitabu cha kumbukumbu cha Nesiya na rafiki zake wakati wa likizo.

TAREHE	MAELEZO	PICHA
9 Juni	*Mimi na rafiki zangu tuliamka mapema sana. Tulioga na kujiandaa kwa safari kutoka Dar es Salaam kwenda Mbuga ya Wanyama ya Tarangire, Arusha, Tanzania. Tulisafiri kwa basi ambayo ni njia ya kusafiri rahisi na ya bei nafuu sana. Njiani tuliona miji na vijiji vingi. Pia tuliona mito, kama vile mto Wami na mto Pangani. Tulipofika Moshi kwa sababu hapakuwa na mawingu, tulipata bahati ya kuuona mlima wa Kilimanjaro. Mlima mrefu kuliko yote Afrika. Tulifurahi sana. Arusha tulilala katika hoteli ya Silver Palm. Ni hoteli nzuri sana, sana, sana, sana!*	
10 Juni	*SIKU YA SAFARI! Tuliamka asubuhi sana kwa sababu wanyama wengi wanaonekana asubuhi. Ilikuwa safari ya saa mbili hivi mpaka katika Mbuga ya Wanyama ya Tarangire. Tarangire kuna tembo wengi kuliko wanyama wengine. Lakini pia tuliona twiga na pundamilia wengi. Kulikuwa pia na swala, nyani, na ndege wengi. Tulipata bahati ya kumwona simba na watoto wake. Tulirudi Arusha na tulipokula tu tulilala kwa sababu tulikuwa tumechoka sana.*	
11 Juni	*Tulichelewa kuamka. Tuliamka saa tatu hivi. Tulikula chamshakinywa, halafu tulitembelea Soko la Wamasai. Tulinunua vitu mbalimbali, pamoja na tisheti, mapambo, viatu, nguo nyingine, na kadhalika. Pia tulitembea mjini; na usiku tulienda disko. Mimi nilicheza sana kwa sababu ninapenda sana muziki. Labda nitakuwa mwanamuziki. Tulilala saa saba usiku.*	
12 Juni	*Tuliamka mapema kwa sababu ni siku ya kurudi Dar es Salaam. Moshi hatukuona mlima Kilimanjaro kwa sababu ya mawingu mengi. Tulilala sana njiani, na tulifika Dar es Salaam saa moja usiku. Kila mmoja alikwenda nyumbani kwao.*	
13 Juni	*SIKU YA KULALA TU kwa sababu ni sikukuu! Nilifurahia sana safari hii, na ninapanga kusafiri kila wakati wa likizo. Mdogo wangu mtundu alinipiga picha nikiwa nimelala!*	

Kutoka *Msafiri – The Traveller, Jumapili* (Juni 2010)